

# MUUNDO WA MPANGO MKAKATI WA TCRA 2021/22-2025/26

## Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

- Kuboresha hali ya maisha ya Watanzania;
- Kujenga utawala bora;
- Kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani kutoka nchi nyingine.

## Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Kuimarisha uwezo wa TEHAMA katika sekta ya uzalishaji na viwanda, kuboresha miundombinu na huduma

## SERA YA TAIFA YA TEHAMA

Mfumo wa kujenga, kusambaza na kutumia TEHAMA kuibadili Tanzania kuwa jamii inayozingatia maarifa kupitia matumizi ya TEHAMA

## ILANI YA CHAMA TAWALA

Umuhimu wa miundombinu ya mawasiliano katika kujenga na kufanikisha uchumi endelevu, kuinua ubora wa malisha na kuimarisha viwango vya maisha ya Watanzania

## MASUALA MUHIMU

- Kupatikana kwa matumizi na unafuu wa huduma za mawasiliano kwa maeneo yasiyo na huduma na ambayo yamefikishiwa huduma pungufu;
- Matukio ya usalama mtandaoni na matumizi yasiyofaa ya mitandao;
- Ufanisi na upatikanaji wa kuaminika wa huduma za mawasiliano;
- Kufuatilia huduma za mawasiliano;
- Ubunifu katika sekta ya mawasiliano;
- Uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango;
- Elimu kwa umma kuhusu masuala ya kidijitali na uelewa wa watumiaji kuhusu huduma za mawasiliano;
- Mifumo na utaratibu unaofanikisha shughuli mbalimbali;
- Tafiti na durusi kuhusu huduma zinazosimamiwa pamoja na teknolojia zinazchipukia;
- Kufanya kazi na wadau kushirikiana na wadau katika kusimamia Sekta ya Mawasiliano.

## DIRA

Jamii ili-yowezeshwa na huduma za kielektroniki na posta zenye hadhi na viwango vya kimataifa

## DHIMA

Kusimamia huduma za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kwa kuendeleza ushindani wenye tija, ufanisi wa kiuchumi na upatikanaji wa huduma bora kwa wote; pamoja na kulinda maslahi ya wadau kwa ustawi wa jamii ya Kitanzania

## MALENGO YA KIMKAKATI

- Miundombinu ya mawasiliano ya kielektroniki na posta zenye ufanisi, inayoaminika na salama, iliyoendelezwa
- Upatikanaji, unafuu na ubora wa huduma za mawasiliano ya kielektroniki na posta uliyoimarishwa
- Huduma zinazosimamiwa, ubunifu, utengenezaji na utoaji wa maudhui ya ndani kwa maeneo husika zilizoimarishwa
- Utendaji na ufanisi wa watoa huduma na kulinda maslahi ya wadau uliyoimarishwa
- Uwezo wa utendaji wa Taasisi uliyoimarishwa

## MIKAKATI

- Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za mawasiliano;
- Kuboresha uendeshaji wa miundombinu ya mawasiliano ya kielektroniki na posta;
- Kuimarisha uwezo wa kusimamia usalama mtandaoni.
- Kuendeleza upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwenye maeneo yasiyo na huduma na yale yenye huduma pungufu;
- Kuendeleza upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano ya kielektroniki na posta;
- Kuimarisha uelewa na elimu kwa umma kuhusu huduma zinazosimamiwa.
- Kuchochea na kuwezesha ubunifu, utafiti na durusi kwenye masuala yanayojitokeza;
- Kuwezesha utengenezaji na usambazaji wa maudhui ya ndani.
- Kuimarisha usimamizi wa utoaji leseni;
- Kuimarisha uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango;
- Kuchochea na kuwezesha ushindani na ufanisi miongoni mwa watoa huduma;
- Kuimarisha utaratibu katika ushirikishwaji wa wadau;
- Kuimarisha uelewa wa umma na elimu kwa umma kuhusu huduma zinazosimamiwa;
- Kuimarisha usalama na ulinzi wa watu kupitia TEHAMA
- Kuendeleza na kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa.
- Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Taasisi;
- Kuimarisha miundo na mifumo ya shughuli za Taasisi;
- Kuboresha mazingira ya kazi;
- Kuendeleza na kuimarisha taswira na hadhi ya Taasisi;
- Kuimarisha upangaji, ufuatiliaji na tathmini.

## MATOKEO YA KIMKAKATI

- Upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroniki na posta imara na za kuaminikana;
- Kuimarika kwa upatikanaji, unafuu na ubora wa huduma za mawasiliano za kielektroniki na posta;
- Jamii yenye uelewa wa masuala la maudhui ya ndani;
- Kuboresha uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo na utendaji wa soko;
- Kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji wa Taasisi.

## LENGO LA MAENDELEO KATIKA SEKTA

Kuimarika na kuendelezwa kwa utoaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroniki na posta kwa wote na kwa gharama nafuu

TUNU: Weledi, Uwezeshaji, Ubunifu, Uadilifu, Uwajibikaji, Kutokubagua